# MTIHANI WA PAMOJA WA MWIGO WA SULIMO
# JULAI, 2024

## KISWAHILI 102/3 FASIHI MWONGOZO

**FASIHI SIMULIZI**

**SWALI LA LAZIMA**

Zimepita siku ayami
Siku chungu tangu giza lipotanda
Wakati lipotazama kwa kiwewe na shauku
Pumzizo kapania, roho kupigania
Ziraili alipokakamaa aushiyo kufakamia.

Nilikwita kwa sauti
Ela penzi hukunitika
Machoyo litunga mbele
Kumkabili huyu nduli
Nikabaki kunyong'onyeya
Jaala kitumainia,
Mtima kujiinamia
Hatima kungojea.

Ya mwisho lipopumua,
Alfajiri ya kiza kikuu
Nlidhani wananichezea,
Mizaha yako kawaida
Lilijaribu kupulizia
Hewa toka langu pafu,
tumaini kiniambia pumzi zangu takuhuisha
Sikujua hizo likuwa juhudi za mfa maji muhebi.

Macho libaki kutunduiya, tabasamuyo kitaraji
Kumbe mwenzangu kaniacha!
Ukiwa ulinivaa, ukungu ukatwandama
Pa kuegema, sikujua fundo chungu linisakama
Tabibu alipoingia na kutangaza rasmi mauko.

Ilikuwa kana kwamba ndo jana lipofunga nikahi.
Kumbukizi zilinijia kwa chozi teletele
Japo kifo ni faradhi ndwele hino halieleweki
Ama jicho la hasadi,
Limekuangaza jamani?



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Koja hili ninalokuwekea,
Kando ya kasri hili la shakawa
Ni hakikisho toka kwangu, nitatambua sana na njia
Kutafuta alotwendea kinyume kutupoka,
Mauko kutuleteya.

Maswali

a. Utungo uliosoma ni mfano wa mbolezi. Thibitisha (al 5)

- ***Siku chungu tangu giza lipotanda***
- ***Pumzizo kapania, roho kupigania***
- ***Nilikwita kwa sauti,Ela penzi hukunitika***
- ***Ziraili alipokakamaa aushiyo kufakamia.***
- ***Ya mwisho lipopumua, Alfajiri ya kiza kikuu***
- ***Kumbe mwenzangu kaniacha***

b. Tambua nafsi neni katika utungo huu (al. 2)
***Mpenzi/mke/mchumba/mume- Ilikuwa kana kwamba ndo jana lipofunga nikahi (2/0)***

c. Jadili vipengele vitatu vya kimtindo katika utungo huu (al3)
mbinu rejeshi- Zimepita siku ayami

- ***jazanda-giza***
- ***taswira-nilikwita kwa sauti***
- ***swali balagha- Limekuangaza jamani?***
- ***Nafsi ya kwanza-nilikwita***
- ***Nahau-funga nikahi***
- ***Tashihisi-ukiwa ulinivaa***
- ***Nidaa-Kumbe ,wenzangu kaniacha!***

d. Umepewa nafasi ya kuwasilisha kipera hiki mbele ya hadhira teule.Eleza sifa zozote tano utakazotumia kufanikisha uwasilishaji wako alama 4

i. ***Ningevaa maleba***
ii. ***Kupaza sauti***
iii. ***Viziada lugha***
iv. ***Kushirikisha hadhira***
v. ***Ujasiri***
vi. ***Aelewe hadhira yake***
vii. ***Awe mbaraza***
viii. ***Aeleze historia, desturi na utamadani/ wa hadhira yake***

e. Kipera hiki kinaendelea kufifia katika ulimwengu wa sasa .Fafanua kwa hoja tatu sababu za hali hii alama 3

i. ***Mwingiliano wa watu/ndoa mesto***
ii. ***Shule za bweni zinawatinga wanafunzi kutotangamana na wanajamii wengine***
iii. ***Fasihi simulizi inaonekana kupitwa na wakati***


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

iv. ***Kutoionea Fahari fasihi simulizi***
v. ***Teknolojia mpya***
vi. ***Kuvumbuliwa kwa kazi ya fasihi Andishi***
vii. ***Mabadiliko katika maisha kwa sababu ya kazi***
viii. ***Ukosefu wa fanani wa kuridhisha kipera hiki.***
ix. ***Uhaba wa watatifiti wa kutosha.***
x. ***Kipera hiki hakidhamini na serikali hivyo kinafifia***

f. Jadili udhaifu wa kutumia mbinu ya kushiriki katika kukusanya data ya utungo huu ⅓
i. ***Makini ya mtafiti yanaweza kutekwa na kusahau kukusanya data***
ii. ***Ni ghali kusafiri***
iii. ***Watu kuogopa kwa kuwepo kwa mgeni***
iv. ***Data inayokusanywa inaweza kuwa ya kutotegemewa kwa kuwa watu wanaweza kuzidisha uwasilishaji wao***
v. ***Kudai malipo.***
vi. ***Hutumia muda mwingi.***
vii. ***Kikwazo cha lugha hutinga mawasiliano.***

**NGUU ZA JADI**

2. "Mwenyezi Mungu ni mwema. Alisikia maombi na kilio chetu. Wanadamu wengine ni maadui wakubwa…"

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
***Haya ni maneno ya Mbungulu. Akimwambia Mangwasha. Wanazungumza wakiwa katika kituo cha kupiga kura. Hii ni baada ya Lonare kupatika na kulazwa hospitalini.***

b) Changanua mtindo katika dondoo hili. (alama 2)
i. ***jazanda-maadui wakubwa***
ii. ***mdokezo-wanadamu wengine ni maadui wakubwa…***
iii. ***taswira-alisikia maombi na kilio chetu***

c) Eleza sifa mbili za msemaji zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)
i. ***Ni mcha Mungu-Mwenyezi Mungu ni mwema.***
ii. ***Mwenye masikitiko-wanadamu wengine ni maadui wakubwa***
iii. ***Mwenye shukrani-anatambua kuwa kuokolewa kwa Lonare ni ombi lililojibiwa.***

d) Jadili ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari katika dondoo hili. (alama 12)
i. ***Sagilu anawapa Watoto maziwa yaliyotiwa sumu na kuwasababishia kuendesha na wengine kulazwa hospitalini.***
ii. ***Chifu Mshabaha ni adui wa mangwasha kwa kumfuta kazi na kumuajiri Mkule mwenzake.***
iii. ***Lesulia ni adui wa Waketwa kwani anawapa wakule kazi pekee yao.***
iv. ***Nanzia ni adui wa wanamatuo wa kufisidi majengo ya umma kama vile Skyline Mall.***
v. ***Mrima ni adui wa waketwa kwa kukubali kuhongwa na Sagilu ili aharibu kura za Lonare.***
vi. ***Cheiya ni adui wa Mashauri kwani alimsaliti kwa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Sagilu.***


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

vii. ***Sagilu ni adui wa Mashauri kwa kumchukua mchumba wake Cheiya.***
viii. ***Sagilu ni adui kwa mkewe kwa kuwa ana uhusiano wa kimapenzi na Cheiya.***
ix. ***Lesulia ni adui wa Lonare kwani anamteka nyara na kujitangaza mshindi wa kiti cha mtemi.***
x. ***Sihaba ni adui wa wasichana kwani anawahusisha katika biashara ya ukahaba badala ya kuwa shuleni.***
xi. ***Mrima ni adui wa Mangwasha na Watoto wake kwani anawasaliti na kupotelea ulevini.***
xii. ***Sagilu anawauzia wanachi bidhaa ghushi***
xiii. ***Sagiluanahujumu biashara za wapinzani wake kama Lonare***
xiv. ***Sagilu anatowesha Mrima kwa kumpa pesa***
xv. ***Lesulia anawalipa vijana ili kuzua vurugu***
xvi. ***Lesulia anamnyang'anya leseni Mafamba na Hakimu.***
xvii. ***Mshabaha anapanga kuteketezwa kwa makazi ya waketwa***
xviii. ***Chifu anamtusi Mangwasha.***
xix. ***Sihab anapeleka kilipuzi katika harusi ya Mangwasha na mrima.***
xx. ***Mashauri anabomoa majengo ya Lonare bila makosa***.

AU

3. (i) Tambua mbinu zozote nane za kimtindo katika dondoo hili. (al. 8

"Very true. Uchumi wa nchi umewatia wengi taflisi. Viongozi wamevimba kichwa. Ninayosoma yote haya katika mitandao ya mawasiliano nikiwa huko ughaibuni.Wamewaacha watu kutumbukia mashimoni na washikilia kukutu kwamba wasalie humo" . "Wamehiari kuwafukarisha ili wazidi kuwatawala. Dunia ya walalaheri hii.Chuma chao ki motoni. Tusubiri tu. Wengine watapigwa na bumbuazi wasalie kuokota taka mitaani." Aliongeza "Wapi! Wengi wao wataabiri vyombo wakimbilie ughaibuni. Watuachie sisi gofu la nchi tusalie kuchinjana tu," alitamka Lombo kwa huzuni. Kisha alimtazama Mashauri kwa muda na Kusema, "Tell me the truth, do you think babangu atashinda? Naonaamekumbwa na pingamizi nyingi. Wapinzani wake…"

a) ***Kuhamisha msimbo- Very true. Uchumi wa nchi umewatia wengi taflisi***
b) ***Nahau-wamevimba kichwa***
c) ***Tanakali za sauti- washikilia kukutu***
d) ***Taswira-wametumbukia mashimoni***
e) ***Jazanda-kutumbukia mashimoni***
f) ***Utabiri/ubashiri/kiona mbele/kisengere mbele- Wengine watapigwa na bumbuazi wasalie kuokota taka mitaani."***
g) ***Nidaa- Wapi!***
h) ***Usimulizi wa nafsi ya tatu- Wengine watapigwa na bumbuazi wasalie kuokota taka mitaani***
i) ***Swali balagha-Tell me the truth, do you think babangu atashinda?***
j) ***Kuchanganya ndimi- Tell me the truth, do you think babangu atashinda?***

ii) Jadili umuhimu wa mandhari ya Ponda Mali katika riwaya Nguu za Jadi. (alama 7)



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

a) ***Inachimuza sifa za mangwasha kama Mwanamapinduzi – anaamua kwenda kinyume***
b) ***na mila na kumtafuta Mrima pale Ponda Mali.pia ni mwenye Mwenye mapenzi,jasiri,***
c) ***na mwajibikaji.***
d) ***Inachimuza mgogoro katika ndoa kwani mrima analewa ponda mali kwa pesa***
e) ***anazopewa na Sagilu huku akitelekeza familia yake katkia umaskini.***
f) ***Dhamira ya mwandishi inakuzwa Athari ya vileo, afya duni, upyaro -mlevi kuimba***
g) ***Maria unanuka kikwapa.***
h) ***Inaendeleza ploti- mangwasha kutongozwa na walevi, Wapishi kupika katika madhari***
i) ***chafu miguu ya ngombe na kanyagio kupikwa kwa pamoja.***
j) ***Inatambulisha wahusika kama Maria, mlevi anayeimba.***
k) ***Endeleza maudhui umaskini ,unywaji pombe, ukiukaji wa haki za Watoto, malezi nk***
l) ***Inachimuza toni ya masikitiko.***
m) ***Mbinu za kimtindo taswira, nk***
n) ***Zingatia vipengee sita kuu hata hivyo akizingatia vingine atuzwe. Zozote 7x1=***

(iii) Jamii ya Matuo katika riwaya ya 'Nguu za Jadi' imekumbwa na usaliti si haba. Kwa kutoaMifano mwafaka riwayani, onyesha ukweli wa kauli hii. (alama 5)

a. ***Chifu Mshabaha anaisaliti jamii ya Waketwa kwa kushiriki katika njama ya kuwaondoa kutoka katika makao yao.***
b. ***Chifu anamsaliti Mangwasha anapompa Mrima bahasha ya pesa kama hongo ya kuendesha kampeni za Mtemi Lesulia,kinyume na matakwa ya jamii yake.***
c. ***Usaliti unaendelezwa na chifu pale anapomsaliti Mangwasha kwa kumleta msichana mwingine kazini kwake ili kumfuta yeye kazi.***
d. ***Maudhui ya usaliti yanajitokeza kupitia kwa Mtemi Lesulia pale anapousaliti uaminifu wa Ngoswe kwa kuwaambia waende kuvuruga amani wakati wa uteuzi wa viongozi ili kuhakikisha ushindi unamwendea Sagilu bila kujali iwapo wangeuliwa na askari.***
e. ***Mtemi anaisaliti nchi pamoja na wananchi wa Matuo kwa kuzorotesha uchumi kupitia kwa sera mbovu za uongozi na ufisadi uliokithiri.***
f. ***Anaisaliti jamii ya Waketwa kwa kuibagua katika ajira, biashara, hata katika makazi yao.***
g. ***Maudhui ya usaliti yanajitokeza kupitia kwa Mtemi Lesulia pia kwani licha ya mwanasheria Mafamba kuifanyia serikali yake kazi na kumfichia uovu wake katika kesi za ufisadi, anamnyang'anya cheti cha uanasheria na kumtowesha kutoka mjini Taria. Pia anamnyang'anya hakimu cheti chake cha uanasheria na kumfuta kazi licha ya kwamba alikuwa akitekeleza majukumu yake kulingana na sheria.***
h. ***Maudhui ya usaliti yanaendelezwa na Sagilu anapoisaliti jamii ya Waketwa walioishi Matango kwa kushiriki katika kuchoma makazi yao licha ya kwamba yeye mwenyewe alitaka achaguliwe kuwa mbunge wao.***
i. ***Sagilu anamsaliti Mrima kwa kumhonga pesa ashiriki katika anasa huku akijua alimtaka Mkewe kimapenzi.***
j. ***Sagilu anamsaliti Mangwasha kwa kumtembelea na kujifanya anayajali maslahi yake ilhali ndiye anayemfadhili Mrima kushiriki ulevi na anasa hadi kufutwa kazi.***
k. ***Sagilu anamsaliti mwanawe Mashauri kwa kumnyang'anya mchumba wake Cheiya bila kujali heshima yake.***


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

*l.* ***Pia anamsaliti Mtemi Lesulia kwa kumhakikishia kuwa kila kitu kiko shwari wakati wa uchaguzi mkuu huku akijua kwamba katu Lesulia hangeshinda katika uchaguzi huo.***
*m.* ***Kupitia kwa Mrima, maudhui ya usaliti yanabainika anapoisaliti jamaa Yake kwa kushirikiana na Sagilu huku mkewe na wanawe wakiteseka.***
*n.* ***Mrima pia anamsaliti mkewe kwa kufanya usuhuba na wanawake nje ya ndoa hasa kupitia kwa barua anayoipata Mangwasha,huku mkewe akijitahidi kuitunza familia bila usaidizi kutoka kwake.***
*s.* ***Usaliti pia unajitokeza pale Mrima anapoisaliti jamii yake hasa Lonare na wengine***
*t.* ***Waliomwokoa kutoka katika maisha ya ulevi, pale anapochukua hongo ili amfanyie mtemi kampeni ilhali akijua huyu alikuwa adui wa Waketwa.***
*u.* ***Maudhui haya pia yanaendelezwa na Cheiya anayemsaliti Mashauri anapokubali kufanya usuhuba na Sagilu bila kujali kuwa huyu alikuwa mzazi wa Mashauri.***
*v.* ***Nanzia anamsaliti mumewe Mtemi Lesulia pale anapofanya usuhuba na Mhindi pamoja na Sagilu na kuzaa watoto nje ya ndoa.***
*w.* ***Usaliti wa Mbwashu unatokea pale anapotorokea Ulaya baada ya Mtemi Lesulia kushindwa katika uchaguzi mkuu. Anamtoroka baada ya kutajirika kutokana na utawala wake huku akimwacha na fedheha ambayo hakutaka kushiriki wala kujihusisha na uovu waliofanya pamoja wakati wa utawala wake.***

**<u>MAPAMBAZUKO YA MACHWEO</u>**

4. **MSIBA WA KUJITAKIA (D.W. lutomia)**

"Mambo yangalifanyika kinyume , basi matopeni ingalikuwa na hadhi tofauti…."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili . (al.4)

*i.* ***Huu ni ujumbe mfupi wa Simu kutoka kwa Kahindi Mlalama.***
*ii.* ***Anamwandikia bwana Fumo.***
*iii.* ***Ni baada ya matokeo ya uchaguzi kutangazwa.***
iv. ***Anampa pole mwenzake kwa vile hakuchaguliwa kuwa kiongozi***. (zote 4x1 =4)

b) Eleza mbinu mbili za lugha katika dondoo hili. (al.2)

*i.* ***Matumizi ya barua fupi ( ujumbe mfupi)***
*ii.* ***Mbinu rejeshi - kuongelea yaliyofanyika ( uchaguzi) (2x1 = 2)***
*iii.* ***Majazi-Matopeni***

c) Jadili umuhimu wa barua ya Bi. Suluhu kwa Bwana Suluhu katika kufanikisha ploti ya hadithi 'Kifo cha Suluhu'. (alama 6)

*a.* ***Kupitia barua hiyo, mgogoro wa ardhi unajengwa kati ya Bw. Suluhu na Mamake Abigael. Anamwuua ili anyakue ardhi hiyo.***
*b.* ***Kupitia barua hiyo, hatima ya mamake Abigael inabainika. Anauawa na Bw.Suluhu kwa vile alitaka kunyakua ardhi ile/ hatima ya vitoto vya wasichana wa chuo kikuu wanaotungwa mimba na Bw. Suluhu.***
*c.* ***Kupitia barua hiyo mustakabali wa maisha ya Suluhu unabainika. Alianza kwa kukata miti na kuuza makaa na hatimaye akaishia kuwa mbunge.***


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

d. ***Kupitia barua hiyo, usuli wa wananchi kukosa maendeleo unajitokeza. Pesa wanazofaa kufanyiwa nayo maendeleo zinafujwa na Bw. Suluhu akishiriki uroda na wanafunzi wa chuo kikuu kando na kulipa deni ya Bw. Ngoma.***
e. ***Kupitia barua hiyo, wahusika kama vile Mamake Abigail na Bw. Ngoma wanakuzwa.***
f. ***Kupitia barua hiyo, utepetevu wa Bi. Suluhu kuhusu malezi ya wanaounajitokeza. Bi. Suluhu anamshutumu mumewe kwa utepetevu.***
g. ***Kupitia barua hiyo, usuli wa Bi. Suluhu kutamauka unajitokeza. Bw. Suluhu anajihusisha na vimada na kujihusisha katika ufuska na wasichana wa chuo kikuu.***
h. ***Barua hiyo ni kipengele cha ploti kwani kupitia kwayo, Bi. Suluhu anaeleza kadhia anayopitia na kutufafanulia kwa nini ametamauka.***
i. ***Kupitia barua hiyo, mgogoro kati ya Bi. Suluhu na nafsi yake unakuzwa. Anatatizika kuhusiana na kutelekezewa jukumu la malezi na Bw. Suluhu Pamoja na mienendo hasi ya Bw. Suluhu.***

Zozote 6x1=6

d) Eleza changamoto zinazowakumba vijana maishani kwa kurelejea: (alama 8)

i. Nilitamani

i. ***Msongo wa mawazo - Tumaini anazongwa na mawazo kutokana na halingumu ya maisha kutoka utotoni.***
ii. ***Kutengana na familia - Tumaini anamwacha mwanawe Radhi na bibi yakeFarida ili kusaka maisha bora ila hafanikiwi.***
iii. ***Kulaghaiwa - Nina anamwonya Tumaini dhidi ya Wabongo wanaoonekanakuwa na umoja na utangamano kumbe wana balaa.***
iv. ***Kukosa nauli - Tumaini anamdanganya utingo kuwa amepoteza kipochichake ila alifanya hivyo ili apate msaada wa kubebwa bila nauli.***
v. ***Tatizo la kuwa mgeni mjini - Tumaini anaogopa kuomba kazi kwa Wahindikwa sababu ya kuongea Kiswahili cha ulimi tofauti na sura yake ya kigeni.***
vi. ***Kukosa msaada mjini - Tumaini anadondokwa na machozi Kariokoo kwakuwa hana mtu wa kumsaidia na hakutaka kumsumbua rafikiye Nina.***
vii. ***Kukosa kuaminiwa -Tumaini anapoomba msaada kwa kijana mmoja anayefanya kazi kwa magari ya Tahmeed, kijana huyo anamuuliza iwapo anamtapeli.***
viii. ***Kufanya kazi duni - Tumaini anataka afanye chochote baada ya kusaka ajira kwa muda mrefu bila mafanikio ili asife njaa.***
ix. ***Kutoweka kwa watu wanaowatolea ahadi za kazi. Kijana anayefanya kazikatika magari ya Tahmeed hakumpigia simu kumfahamisha iwapoamepata kazi jinsi alivyomwahidi au la na Tumaini anapompigia simu anamkosa.***
x. ***Kukata tamaa - Tumaini anasema kuwa anahitaji kuchukua hatua nyinginekwa kuwa ya ajira yameshindikana.***
xi. ***Hofu ya kurudi nyumbani mikono mitupu. Tumaini anashangaa akirudi nyumbani Kenya atarudi na nini ilhali hana chochote. Anashangaa jinsi ambavyo atapokelewa na bibi yake.***
xii. ***Kukumbwa na njaa - Tumaini anafika mjini Kigamboni akiwa na njaa kwa kuwa siku iliyotangulia hakuwa ametia chochote tumboni isipokuwa chai ya rangi aliyoinywa usiku.***


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

xiii. ***Anasa - Tumaini anasema kuwa anataka gari ili ataabishe mji.Vijana ni wepesi wa kushawishika. Tumaini anapomwona Romeo anampenda wakati huo huo kwa kuwa ni mtanashati na ana gari japo hamfahamu vyema.***
xiv. ***Mapuuza - Tumaini anapuuza ushauri wa Nina dhidi ya kujihusisha na Wabongo na anaponea chupuchupu kutolewa kafara na Romeo.***
xv. ***Tamaa ya mali - Tumaini anataka awe na gari la kifahari,majumba mazuri ya kukodisha, mashamba kama alivyo Nina bila kujua ni vipi atavipata vitu hivi.***
xvi. ***Tamaa ya mume tajiri - Tumaini anatamani mume aliye na mali ndiposa anashawishika kwa upesi na Romeo anayetaka kumtoa kafara.***
xvii. ***Kukumbwa na wivu - Tumaini anamwonea wivu Nina kwa kuwa ana mume mzuri na mwenye mali na anakiri kumwonea gere Nina.***
xviii. ***Kutekwa nyara - Tumaini anatekwa nyara na Romeo anayetaka kumtoa kafara.***
xix. ***Usaliti kutoka kwa marafiki - Jenifa anaishiwa na furaha na anaanza kumnunia Tumaini amabaye ameishi kwake kwa muda. Tumaini anaamini kuwa hali hii inatokana na yeye kutumia vitu vyae pale nyumbani.***
xx. ***Kuwa wategemezi - Tumaini anawategemea marafiki kama vile Nina kwa makazi na chakula na sasa hana amani na anaondoka kwa Nina ili aweze kujitegemea.***
xxi. ***Uchovu wa kutembea sana mjini - Tumaini anatembea mjini kutoka asubuhi hadi adhuhuri, hili linamfanya kuchoka sana.***

ii. Mapambazuko ya Machweo na hadithi nyingine

i. ***Kukosa kazi-sai na dai***
ii. ***Mishahara duni***
iii. ***M,azingira duni***
iv. ***Kukatizwa elimu***
v. ***Kutishwa na walinzi***
vi. ***Kunyimwa uhuru wa kutembea***
vii. ***Kutenganishwa na familia***
viii. ***Kufanyinshwa kazi ya sulubu***
ix. ***Ukosefu wa mavazi***
x. ***Mihadarati***
xi. ***Ajira kutolewa kwa mapendeleo.***

**5. HADITHI FUPI**

NIPE NAFASI

"Walitaka kuelewa kuwa mume kuwa na wake wengi ilikuwa ni jambo la kawaida, jambo ambalo 'mke mwema' hakufaa kulalamika."

a) Tambua mbinu tatu za kimtindo katika dondoo hili. (alama 3)

i. ***Kinaya- Walitaka kuelewa kuwa mume kuwa na wake wengi ilikuwa ni jambo la kawaida, jambo ambalo mke mwema hakufaa kulalamika***
ii. ***Mbinu rejeshi- Walitaka kuelewa kuwa mume …***
iii. ***Takriri-jambo***
iv. ***Usimulizi-walimtaka kuelewa kuwa mume kuwa…***
v. ***Kejeli-'mke mwema'***



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

b)Mrejelewa wa kauli hii alifaa kulalamika. Thibitisha. (alama 7)

i. ***mama mkwe kutumiwa pesa***
ii. ***moshe kutelekeza familia yake***
iii. ***mama kazili kuachiwa jukumu la kuwalea Watoto pekee yake***
iv. ***alitakiwa kuomba ruhusa ya kutafuta kazi.***
v. ***Kuomba ruhusa ya Kwenda kwa jamaa yake***
vi. ***Kutofikishiwa pesa za matumizi na mama mkwe.***
vii. ***Kutoruhusiwa kujitetea mbele ya kraal***
viii. ***Kunyimwa uraia wa Lesotho***
ix. ***Kushurutishwa kurudi kwao***
x. ***Kulaumiwa kwa kifo cha mkathini***
xi. ***Kupinga uamuzi wa kraal***

c) Jadili changamoto zinazokumba mtoto wa kike katika hadithi ya 'Sabina.' (Alama 10)

i. ***Sabina anafiwa na mama na nyanya/babu.***
ii. ***Sabina anafanyishwa kazi nyingi kama vile, kuuza maziwa***
iii. ***Sabina anakosa nafasi ya kudurusu***
iv. ***Sabina anamtelekezwa na Yunuke***
v. ***Sabina anadharauliwa na Yunuke na Ombati***
vi. ***Sabina anatukanwa na Yunuke.***
vii. ***Sabina anapigwa na Yunuke bila sababu.***
viii. ***Kubaguliwa kwa sabina-hakuruhusiwa Kwenda shule ya bweni.***
ix. ***Nyaboke kupata ujauzito mapema.***
x. ***Sabina anakosa mavazi/sare bora***
xi. ***Nyaboke na sabina wanaoneka kama kitegauchumi***
xii. ***Ndoa za lazima-Sabina.***
xiii. ***Sabina anakosa malezi ya baba.***
xiv. ***Nyaboke anasalitiwa na babake Sabina.***

**BEMBEA YA MAISHA**

6. ***Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:***

"Eti hajakosa adabu? Mtu ana ubaguzi kama nini! Ana moyo mgumu kama jiwe. Amejaliwa lakini bahili kama mchanga wa dhahabu. Hajui mali ya bahili huliwa na wadudu?"

a)Eleza muktadha wa dondoo hili (alama4)

- ***Msemaji ni Asna***
- ***Msemewa ni Sara na Neema (akitaja Sara pekee yake mpe)***
- ***Wako hospitalini***
- ***Sara amejibu kauli ya Asna kwa kusema kwamba Bunju hajakosa adabu ndipo Asna akasema hayo. Baadaye, Sara anamtahadharisha Asna kwamba akiendelea kumhukumu Bunju atamvunjia Neema ndoa***

b)Tathmini umuhimu wa maswali balagha katika dondoo hili (alama2)

- ***Eti hajakosa adabu? ~ kuonyesha kutokubaliana na jambo…***
- ***Hajui mali ya bahili huliwa na wadudu? ~ kusuta/Kukejeli***



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

c)Toa mifano ya vipengele vingine viwili vya kimtindo katika dondoo hili (alama4)

- ***Tashbihi ~bahili kama mchanga wa dhahabu, moyo mgumu kama jiwe***
- ***Kinaya ~ Bunju kufanikiwa lakini anakosa kusaidia***
  ***~Sara kusema kuwa Bunju hana makosa ilhali amekataa Sara aishi kwake.***
  ***Methali ~ mali ya bahili huliwa na wadudu***
  ***Chuku ~ binadamu kusemekana kuwa na moyo mgumu kama jiwe(si jambo la kawaida)***

d)Fafanua nafasi ya anayeitwa bahili katika dondoo hili kwa kuijenga tamthilia ya Bembea ya Maisha (alama10)

***Umuhimu wa Bunju***

- ***Anatumiwa kukuza mgogoro kati ya usasa na utamaduni. Kushikilia utamaduni***
- ***kunamfanya azozane na Neema ambaye anaamini kwamba mambo yamebadilika, hakuna ubaya wa kuishi na mama yake kwao.***
- ***Anaendeleza ploti. Kumwokoa Neema kunabadilisha mkondo wa hadithi. Anakuja kumwoa Neema.***
- ***Anaendeleza maudhui mbalimbali kama vile utu. Anamwokoa Neema***
- ***Anakuza sifa za wahusika wengine. Kupitia kwake, tunaona ujasiri wa Neema. Neema***
- ***anamkabili na kumwambia kwamba anakasirika bure. Anamwonyesha haja ya kusem wazi atakalo badala ya kunyamaza.***
- ***Ametumiwa kuonyesha changamoto zinazokumba malezi. Yeye na mkewe hawana muda wa kumpeleka Lemi out kwa sababu ya kazi. Analalamika kwamba mkewe amemwachia kazi ya malezi. Yeye ndiye anayemsaidia Lemi kufanya homework.***
- ***Anaendeleza suala la utabaka. Jumba analoishi lina nafasi kubwa ikilinganishwa na chumba kimoja ambamo Asna anaishi***
- ***Anakuza mbinu jereshi kwa kurejelea wazazi wake walipokuwa hai.***
- ***Anakuza neema kuwa mbishi***
- ***Anatambulisha wahusika kama vile wazazi wake.***
- ***Anakuza toni ya dharau na ukali anapozua mgogoro na Neema***
- ***Ni mfano wa wanaume wanaowapa wake wao fursa ya kujiendeleza kwa kuachia neema mshahara wake.***
- ***Anakuza dhamira ya mwandishi kwa kuonyesha changamoto zinazokumba asasi ya ndoa.***

7. a) Kila binanadamu hukabiliana na mabadiliko katika maisha yake.
   Jadili kauli hii ukirejelea tamthilia ya Bembea ya maisha. ( al.10)

   **Majibu**

- ***Kutoka ujana hadi uzee-Yona Sara,***
- ***Sheria kubadilika-katika elimu-huwezi kumnyoosha mtoto kwa kiboko.***
- ***Kubadilika kwa mtazamo-Yona-kuelewa kuwa sara alikua mgojwa.***
- ***Kubadilika kwa hisia-Yona analalamika kwa sara kutopika,baadaye ana mhurumia.***
- ***Yona alikuwa miongoni mwa vijana wa kwanza kutumika kanisani kisha baadaye anakumbatia pombe.***
- ***Yona alikua mzuri mwanzoni,lakini baada ya kusutwa na kudharauliwa alibadilika.***
- ***Yona anasuta kwa kuwa mlevi-anabadilika***



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

- ***Kuna mabadiliko kuhusiana na mila na desturi-kuhusu mtoto wa kike na kiume***
- ***Katika kizazi cha loe,mtoto wa kike anawenza kurithi mali nakushughulikia wazazi***
- ***wake.***
- ***Ndoa inakumbwa na mabadiliko-mtu anachagua wakati wa kuoa/kuolewa/awali***
- ***msichana alilazimishwa.***
- ***Majukumu yamebadilika –Yona anaingia jikoni kupika.***
- ***Mbeleni wazee walifunzwa na dunia-kizazi cha leo kinatengemea vitabu.***
- ***Hali ya uchumi inabadilika-wanaotegemea mifuka yao watakabiliana na kipindi***
- ***kigumu.***
- ***Midindo ya nyimbo imebadilika.***
- ***Burudani – watoto wa kisasa hupenda kupelekwa "out"***
- ***Elimu ya kisasa haina mafundisho kwavijana kuhusu ndoa.***
- ***Mbeleni watoto walifunzwa na kushikilia mila na desturi-sasa wamenzitupa.***
- ***Watoto walitumia lugha asilia , leo hawajui hata neno moja.***
- ***Zamani wasichana hawakupendelea masomo***
- ***Safari za kuenda kijijini hazibughudhi kama zamani kutokana mabadiliko ya***
    - ***kiteknolojia***
- ***Mazao yalikua mengi hapo zamani , sasa mashamba yamedidimika.***
- ***Awali Sara alikuwa mwenye afya na sasa anauguza ugonjwa wa moyo.***
- ***Awali yona alikuwa Mwalimu hodari kisha anakumbatia ulevi na kufutwa kazi.***

***(zozote 10x1 = 10)***

b) Huku ukitoa mifano mwafaka, kutoka katika tamthilia ya bembea ya maisha, onyesha jinsi mbinu rejeshi ilivyojitokeza. (alama 10)

- ***Sara alinyimwa nafasi ya kuendelea na masomo.***
- ***Bunju aklivyomuokoa neema kutoka ajalini***
- ***Sara alikuwa akiwajibika kabla ya kuugua-hakufanya ajizi.***
- ***Sara alilazimika kufanya kazi ili kuwalipia karo Watoto wake.***
- ***Yona alikuwa alihudumu kanisani kabla ya kuwa mlevi***
- ***Yona alifika shuleni mapema na kuwaadhibu waliofika baada yake.***
- ***Yona kueleza maisha ya babake Kalasinga***
- ***Neema anakumbuka jinsi Yona alivyokuwa akiwaadhibu.***
- ***Dina kusimulia maisha ya awali ya sara.***
- ***Sara kusemwa kwa kukosa mtoto.***
- ***Neema kuwa wembe shuleni***
- ***Sara kufunzwa jinsi ya kutunza ndoa yake.***
- ***Yona alikuwa wa kwanza kuhitimu***
- ***Bunju alikuwa na miadi na rafikiye waliyesoma naye.***


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

## 8. USHAIRI

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Daima alfajiri na mapema
Hunipita na jembe na kotama
Katika njia iendayo kondeni
Kama walivyofanya babuze zamani
Nimuonapo huwa anatabasamu
Kama mtu aliye na kubwa hamu
Kushika mpini na kutokwa na jasho
Ili kujikimu kupata malisho.
Anapotembea anasikiliza
Videge vya anga vinavyotumbwiza
Utadhani huwa vimemngojea
Kwa usiku kucha kuja kumwimbia;
Pia pepo baridi kumpepea
Rihi ya maua zikimletea
Nao umande kumbusu miguu
Na miti yote hujipinda migongo;
Kumpapasa, kumtoa matongo;
Na yeye kuendelea kwa furaha
Kuliko yeyote ninayemjua
Akicheka ha ha ha ha ha ha…

Na mimi hubaki nikijiuliza
Kuna siri gani inamliwaza?
Au ni kujua au kutokujua?
Furaha ya mtu ni furaha gani?
Katika dunia inayomhini?
Ukali wa jua wamnyima zao.
Soko la dunia lamkaba koo;
Dini za kudhani zamsonga roho
Anayalimia matumbo ya waroho
Kuna jao gani linamridhisha?
Laiti angalijua, laiti angalijua!

**Maswali**

(a) Fafanua hali ya mzungumzaji katika shairi hili. (alama 4)

- ***i) Ni mwenye bidi- alfajiri na mapema, kutokwa na jasho***
- ***ii) Ni mwenye tumaini/tamaa/hamu kubwa***
- ***iii) Mwenye kufurahia mandhari-anapotembea anasikiliza videge…***
- ***iv) Mtulivu-kuna siri gani inamliwaza?***
- ***v) Anayedhulumiwa- soko la dunia lamkaba koo***
- ***vi) Anayesagika kwa kazi ngumu kuwafaidi wenye tamaa-anayalimia matumbo ya waroho***


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

*vii) Ameridhika -kuna jambo gani linamridhisha?*
*viii) Ni mwenye tabasamu aendapo kazini.*
*ix) Amesongwa roho na dini za kudhani*
*x) Anafanyia kazi matumbo ya waroho.*
*zozote 4x1= 4*

(b) Fafanua aina tatu za taswira ukiurejelea ubeti wa pili. (alama 3)
i) ***Taswira mnuso-rihi yam aua***
***ii) Taswira mguso-kumpapasa, kumbusu miguu***
***iii) Taswira ya usikivu-anasikiliza videge***
***iv) Taswira mwendo- yeye kuendelea kwa furaha***
***Za kwanza 3x1=3***

(c) Bainisha nafsi neni katika shairi hili. (alama 1)
***Mtu anayemtazama mkulima akipita/mtetezi wa haki/anayelalamikia dhulima ya wanyonge. 1x1=1***

(d) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)
***i) Toni ya kuajabia/ kushangazwa na jambo-kuna jambo gani linamridhisha?***
***ii) Toni ya kuhuzunisha/kuhurumia/ kusikitisha- ukali wa jua wamnyima zao.***
***iii) Toni ya uchungu- furaha ya mtu ni furaha gani katika dunia inayomhini?***
Kutaja 1 kueleza 1=2

(e) Bainisha vipengele vinne vya kimtindo katika shairi hili. (alama 4)
***i) Tashihisi***
- ***Umande kumbusu miguu***
- ***Miti yote hujipinda migongo kumpapasa na kumtoa matongo***
- ***Katika dunia inayomhini***
- ***Soko la dunia lamkaba koo***

***ii) Kinaya- mzungumziwa ni mwenye furaha katika dunia inayomhini/ anafanya kazi isiyomfaidi; inafaidi wengine.***
***iii) Tashibihi-huwa anatabasamu kama mtu aliye na kubwa hamua***
***iv) Tanakali- akicheka ha ha ha ha ha ha…***
***v) Nidaa- laiti angalijua! 4x1=4***

(f) Pambanua muundo wa shairi hili. (alama 4)
***i) Idadi ya mizani inatofautiana-***
***ii) Vina vinatofautiana***
***iii) Lina beti nne***
***iv) Kila ubeti una idadi tofauti ya mishororo na beti nyingine***
***v) Kila mshororo una mgao mmoja/ kipande kimoja isipokuwa ubeti wa pili mshororo wa tisa ulio na migao miwili***
***vi) Kiishio kinatofautiana katika kila ubeti. 4x1=4***


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

(g) Eleza umuhimu wa maswali balagha katika shairi hili. (alama 3)

- ***i) Kudadisi hali/ kuonyesha mshangao- kuna siri gani inayomliwaza?***
- ***ii) Kuonyesha hali ya kinyume/kutokubaliana na jambo-furaha ya mtu ni furaha gani, katika dunia inayomhini?***
- ***iii) Kuzindua-furaha ya mtu ni furaha gani katika dunia inayomhini?***
- ***iv) Kuvutia hadhira kwa kuamsha shauku ya msomaji ajihusishe zaidi na shairi husika.***
- ***v) Kufichua uhalisia -kwa kuibua ukweli kuhusu masuala ya kijamii k.v kukata tamaa.***
- ***vi) Kuongeza msisitizo-kuimarisha ujumbe wa mshairi. 3 x 1=3***

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes